PRIMARY END TERM 3 EXAMS
2016

KISWAHILI
STD 6

,
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

KISWAHILI

MUDA: SAA1 DAKIKA40

Soma vifungu vifuatavyo kisha ujaze nafasi zilizoachwa kuanzia 1 - 15.

Si jambo ____1____ ajabu unapotembea ____2____ kwa watu kuwakuta maajuza na ____3____ na wajukuu wao au wanawali na masomo ____4____ wakitaniana kadri mila zinavyoruhusu na pengine mashababi na marika zao wamebarizi ____5____ mabaraza ____6____. Kadhalika ukipita risani utawapata ____7____ na wana wao na hata mashoga wakifanya maongezi. ____8____ maisha yana ____9____ na watu wenye silika ____10____.

1.	A. wa	B. za	C. la	D. ya
2.	A. mastakimu	B. mastikimuni	C. mastikimu	D. mastakimuni
3.	A. mashaibu	B. sahibu	C. masibu	D. masaibu
4.	A. mwao	B. kwao	C. chao	D. zao
5.	A. kuwa	B. zenye	C. kwenye	D. kwa
6.	A. wakinguruma	B. wakipiga gumzo	C. wapiga soga	D. wapiga shoga
7.	A. wavyele	B. wanawake	C. waviele	D. wavee
8.	A. aliangua	B. aliamua	C. almuradi	D. alijua
9.	A. ubaya	B. magumu	C. mazingira	D. mosi
10.	A. kali	B. mbalimbali	C. nzuri	D. balibali

Mgeni ____11____ bwana Afya kumaliza, afisa wa afya wilayani bwana Usafi na hadhirini yote ____12____? Ninachukua fursa hii kuwakaribisha ____13____ skulini kwa ____14____ ya kuchangisha hela za kujenga bwalo. Chambilecho wahenga, kichango ni ____15____.

11.	A. mheshimiwa	B. mkarimiwa	C. mwenzetu	D. mweshimiwa
12.	A. shikamoo	B. habari	C. hamjambo	D. alamsiki
13.	A. humo	B. hapo	C. huko	D. hapa
14.	A. dhumuni	B. mathumuni	C. madhumuni	D. makusudini
15.	A. kutoa pesa	B. kuchangizana	C. kuchangisha	D. kuchanga

Kutoka swali la 16 - 30, jibu kila swali kulingana na maagizo.

16. Ukimwi _____ ugonjwa ulio na watu wengi.
A. ndizo
B. ndio
C. ndiyo
D. ndiwo

17. Kanga ni aina ya ndege. Maana nyingine ya kanga ni
A. madoadoa
B. leso
C. kuku
D. unga

18. Andika kwa wingi
Karatasi imeraruka.
A. karatasi zimeraruka
B. karatasi imetaruka
C. makatarasi zimetaruka
D. makaratasi yameraruka

19. Kinyume cha anika ni
A. anuka
B. funika
C. funua
D. anua

20. Salamu za kuagana usiku ni
A. sabalkheri
B. alamsiki
C. jambo
D. masalkheri

21. Kitendo cha kuku cha kutoa vifaranga kutoka katika mayai ni kutotoa au
A. kuengua
B. kuangua
C. kuagua
D. kuungua

22. Umbo hili laitwaje?

A. Mche
B. Mstatili
C. Mraba
D. Duara dufu

23. Mpunga huzaa
A. mtofaa
B. mchele
C. nazi
D. wali

24. Tarakimu kabla ya 200000 kwa maneno ni
A. Mia moja tisini na tisa elfu mia tisa tisini
B. Laki moja mia tisa
C. Mia moja na tisini na tisa elfu mia tisa tisini na tisa
D. laki mbili

25. Mtu anaye amelemaa mguu mmoja ni
A. matege
B. kiguru
C. kipofu
D. kiwete

26. Andika akisami ifuatayo kwa maneno $\frac{3}{7}$.
A. Tusui tatu
B. Subui saba
C. Thuluthi saba
D. Subui tatu

27. Kukata miti ili iwe mifupi ni
A. kufyeka
B. kupogoa
C. kupalilia
D. kung'oa

28. Tumia _____ ote kwa usahihi
Duniani _____ kunapendeza.
A. mwote
B. kote
C. chote
D. kwote

29. Ni nini maana ya semi kupigwa kalamu.
A. Fanya kazi ngumu
B. Kuandika
C. Achiswa kazi
D. Kupigwa na kalamu

30. Kamilisha sentensi kwa kivumishi sifa sahihi jiwe hili ni
A.ndogo
B. mdogo
C. dogo
D. kidogo

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu swali la 31 - 40.

Hapo zamani za kale paliishi mvuvi mlalahoi. Kila uchao alipoenda kuvua samaki, alifanikiwa kupata samaki mmoja tu. Pesa alizopata kutokana na uvuvi alizitumia kununua nguo na chakula. Hata hivyo wakati mwingine alipata mapato ya kijungu jiko.

Mvuvi huyu alikuwa **mcha Mungu**. Kila mawio aliomba Jalali amkumbuke na kumpa **riziki** yake.

Siku moja alimwomba Mola ampe samaki wengi ili aweze kuuza apate pesa akimu mahitaji yake. Alijua kwamba mcha Mungu si mfaki. Aliingia katika dau lake akaenda baharini kuvua. Alipotupa wavu wake alinasa kitu kizito. Alijawa na bashasha akidhani kuwa alikuwa ameshika samaki wengi.

Alipovuta wavu wake, aliona kwamba alikuwa amewanasa samaki wadogo kama dagaa. Mvuvi huyu alimuna akataka kuwarudisha samaki hao. Kijisamaki kimoja kilimwambia, "Tafadhali mvuvi usiniue. Hata kama mimi ni mdogo, huenda nitakufaa. Twende katika nchi kavu nitakusaidia."

31. Anayezungumziwa alikuwa
A. tajiri
B. fukara
C. mfuasi
D. bwenyenye

32. Mvuvi aliomba Mungu
A. atajirike
B. awe maskini
C. apate samaki wengi
D. anunue nguo

33. Mvuvi alikuwa na mazoea ya
A. kupata samaki mmoja
B. kupata samaki wadogo
C. kula samaki
D. kuvua samaki usiku

34. Kuwa **mcha Mungu** ni
A. kuchezea Mungu
B. kumwomba na kuheshimu Mungu
C. kwenda kanisani
D. kusaidia watu wa Mungu

35. Samaki wengi huitwa?
A. Kikosi
B. Kishazi
C. Halaiki
D. Chane

36. Udogo wa samaki ni kijisamaki je ukubwa ni
A. kisamaki
B. lisamaki
C. jisamaki
D. samaki

37. Kwa nini mvuvi alifurahi?
A. Alifikiri kwamba alinasa samaki wengi
B. Alifikir alimpata samaki mkubwa
C. Alimpata samaki mdogo
D. Samaki waliongea

38. Mvuvi alitumia chombo kipi?
A. Mashua
B. Dau
C. Meli
D. Mtumbwi

39. Ajabu ya samaki walionaswa ni kwamba
A. mmoja wao aliongea
B. walikuwa wadogo sana
C. walivuliwa kwa wavu
D. walikuwa wengi

40. Neno riziki lililopigwa mstari lina maana gani?
A. Mapato ya kila siku
B. Hatari kubwa
C. Chakula
D. Samaki wengi

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 - 50.

Manufaa ya miti ni mengi, hasa kwamba binadamu wa wanyama pia; lakini jambo la kustaajabisha ni yuyu huyu mwanadamu ambaye hufaidika zaidi ndiye hukata miti ovyoovyo kwa ajili ya maslahi yake binafsi.

Miti hutupa vyakula. Sisi hupata vyakula kwa njia ya matunda, mboga na hata mizizi kama vile mihogo. Ipo miti inayotupatia dawa. Mti maarufu sana ni ule wa mwarubaini ambao unasemekana unatibu maradhi arubaini. Mnahara hutibu pumu, mlama ni dawa ya sumu ya nyoka, mkarafuu ni kwa jino au tumbo linapouma na kuna mshubiri unaotibu maradhi kadhaa.

Kuna pia miti ya manukato kama vile muasumini, mwaridi, mkadi na mlangilangi. Miti hutupa vivuli na mbao ambazo zinazotumiwa kwa manufaa mbalimbali.

Wanyama nao hufaidika kwa namna zao. Wako wanaishi wakitegemea miti kama chakula chao kama vile ndovu na twiga. Chui, nyoka na nyani nao huishi mitini na kuifanya majumba yao maficho. Ndege na wadudu pia hufaidika.

Miti inapokatwa basi ni wazi kwamba tunataka kujinyima neema zote hizi mbali na kukimbiza mvua. Atakayeumia zaidi mwishoni ni mwanadamu, maana bila miti au mimea maisha yake yako gizani.

41. Ni kweli kusema kuwa
A. miti hutupa vyakula na dawa pekee
B. mzizi ya miti haina faida yoyote
C. mshubin hutibu maradhi kadhaa
D. mlama ni dawa ya meno

42. Binadamu hukata miti kwa sababu gani?
A. Kuwaondoa nyani mtaani
B. Manufaa yake
C. Kuwakimbiza nyoka
D. Mti humletea shida

43. Kulingana na kifungu ni jambo gani ambalo si la kweli?
A. Wanyama hufaidika sana kutokana na miti
B. Mti humpa binadamu chakula
C. Miti huwafaidi binadamu pekee
D. Miti ina faida kwa binadamu pekee

44. Manukato hutumiwa kwa
A. kunuka
B. kufukuza wadudu
C. kufanya kitu au mtu kunukia vizuri
D. kula

45. Miti inapokatwa, tunajinyima nini?
A. Maji tu
B. Neema na mvua
C. Magonjwa
D. Mazao

46. Wanyama wanaoishi mitini na kufanya majumba yao au maficho ni _____ na _____.
A. ndovu, twiga
B. chui, nyoka
C. ndege, nyani
D. mbuzi, kuku

47. Mti wa mwarubaini hutibu magonjwa mangapi?
A. Robo
B. Mengi
C. Arubaini
D. Sitini

48. Mti unaotusaidia kuondoa sumu ya nyoka ni
A. mnaraba
B. mshubiri
C. mkarafuu
D. mlama

49. Anayejulikana kwa kuikata miti ovyoovyo ni
A. Mungu
B. wanyama
C. binadamu
D. mkarafuu

50. Anwani inayofaa kwa kifungu ulichokisoma ni
A. Manufaa ya miti
B. Mti shambani
C. Hasara za miti
D. Haki za miti